Reli na Matukio Gazeti

Toleo Maalum
Machi 26, 2020

# WATUMISHI WA TRC WALIOFARIKI KATIKA AJALI MKOANI TANGA WAAGWA RASMI



*Majeneza yenye miili ya watumishi watano wa Shirika la Reli Tanzania waliopoteza maisha katika ajali mkoani Tanga yakiwa katika sehemu maalum kwa ajili ya kuagwa na kutolewa heshima za mwisho.*

Miili ya wafanyakazi watano wa Shirika la Reli Tanzania – TRC waliofariki kutokana na ajali ya treni ya uokoaji kugongana na Kiberenge katika eneo lililopo kati ya stesheni ya Mwakinyumbi na Gendagenda mkoani Tanga imeagwa rasmi katika hospitali ya Lugalo jijini Dar es Salaam Machi 24. 2020.

Zoezi hilo la kuaga miili ya mashujaa hao limesimamiwa na uongozi na wafanyakazi wa TRC na kuhudhuriwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Prof. John Wajanga Kondoro na mjumbe wa Bodi hiyo Ndugu Wolfgang Salia, ndugu wa marehemu, Katibu wa Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Ndugu Humphrey Polepole, pamoja na wadau wengine wa TRC wakiwemo Benki ya CRDB, TIB, NBC, wadau wa reli kutoka TAZARA, YAPI MARKEZI pamoja na wadau kutoka chuo cha DIT, Mwakilishi kutoka Clouds Media Group na Meneja kutoka kampuni ya Wasafi Classic Baby (WCB) Ndugu Hamis Taletale maarufu kama Babu Tale.

Mkurugenzi mkuu wa TRC ndugu Masanja Kungu Kadogosa amesema kuwa amesikitishwa na tukio hilo kwani TRC pamoja na Serikali kwa ujumla imepoteza nguvu kazi ambayo ilikuwa ikitoa mchango mkubwa katika Shirika na Serikali.

"Kiukweli nimeumia sana na sijawahi kuumia kama hivi, ila sisi ni wanadamu na chochote kitakachotokea huwa ni mipango yake Mungu, kinachotakiwa ni kushukuru na kuwa na subira" alisema Ndugu Kadogosa.

Aidha, Ndugu Kadogosa amesisitiza kuwa uchunguzi wa chanzo cha ajali hiyo utafanyika kupitia tume huru itakayoundwa hivi karibuni kama ilivyoagizwa na Naibu waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi Mhe. Atashasta Nditiye alipotembelea eneo la ajali hivi karibuni ambapo tume hiyo itatakiwa kutoa majibu ndani ya siku saba tangu kuundwa kwake.

Kadogosa ameongeza kuwa majibu ya uchunguzi huo yatabaini chanzo cha ajali na lengo ni kuepusha madhara kama hayo yasijirudie tena kwani kazi za reli bado zinaendelea na juhudi za kuwalinda wafanyakazi zinatakiwa kufanywa kwani wao ndio nguvukazi ya shirika

Reli na Matukio Gazeti
Toleo Maalum
Machi 26, 2020

# WATUMISHI WA TRC WALIOFARIKI KATIKA AJALI WAAGWA RASMI

Inatoka Uk. 1

na taifa kwa ajili ya kuleta maendeleo kupitia miundombinu ya reli.

TRC imesimamia shughuli zote za mazishi nyumbani kwa marehemu hao ikiwemo katika usafirishaji wa miili, chakula, pamoja na kutoa na kupokea salamu za rambirambi kutoka kwa wadau mbalimbali waliojitokeza na katika maombolezo hayo.

Aidha Ndugu na jamaa wametoa shukurani kwa uongozi na wafanyakazi wa TRC kwa kuweza kushiriki nao bega kwa bega katika kuhakikisha wapendwa wetu wanahifadhiwa katika nyumba zao za milele.



*Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi TRC Prof John Kondoro akitoa salamu za rambirambi kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi TRC kwa wafiwa.*

## KATIKA PICHA TOFAUTI NI BAADHI YA WAOMBOLEZAJI WAKIWA WAMEBEBA MAJENEZA KUELEKEA ENEO LA KUAGA NA KUTOA HESHIMA ZA MWISHO











# MATUKIO KATIKA PICHA WAKATI WA KUAGA MIILI YA WATUMISHI WA TRC WALIOFARIKI KATIKA AJALI MKOANI TANGA



*Katibu wa itikadi na Uenezi CCM Ndugu Humprey Polepole akitoa salamu za Rambirambi katika hafla ya kuaga miili ya wafanyakazi wa TRC kwa niaba ya Chama cha Mapinduzi katika Hospitali ya Lugalo Dar es Salaam Machi 24, 2020*



*Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Ndugu Masanja kadogosa akitoa neno la mwisho na salaam za rambirambi kwa niaba ya uongozi na wafanyakazi wa Shirika wakati wa hafla ya kuaga miili ya wafanyakazi waliofariki katika ajali ya treni, katika Hospitali ya Lugalo jijini Dar es Salaam, Machi 24, 2020.*



*Mkuu wa Chuo cha DIT Prof. Preksedi Ndomba akitoa salamu za rambirambi katika hafla ya kuaga miili ya wafanyakazi waliofariki katika ajali ya treni, katika Hospitali ya Lugalo Dar es Salaam Machi 24, 2020.*



*Meneja Mradi Tanzania kutoka Yapi Merkezi Ndugu Fuat Kamel kwa niaba ya wafanyakazi wa Yapi Merkezi akitoa salamu za rambirambi kwa wafiwa katika hafla ya kuaga miili ya wafanyazi wa TRC waliopoteza maisha katika ajali.*



*Sheikh Issa Abdallah akifanya Dua ya Maombolezo katika hafla ya kuaga miili ya wafanyakazi wa TRC waliofariki katika ajali ya Treni mkoani Tanga, katika Hospital ya Lugalo jijini Dar es Salaam Machi 24, 2020.*



*Mwakilishi wa familia ya Marehemu Geogre Urio akitoa Shukurani kwa Uongozi wa TRC kwa niaba ya familia za wafiwa kwa jitihada walizozifanya tangu kutokea kwa ajali kati ya stesheni ya Gendagenda - Mwakinyumbi mpaka kufikia siku ya kuaga miili ya wafanyakazi hao wa TRC waliopoteza maisha.*

Reli na Matukio Gazeti

Toleo Maalum
Machi 26, 2020

# MATUKIO TOFAUTII KATIKA PICHA WAKATI WA KUAGA MIILI






*Waombolezaji wakiongozwa na uongozi wa Shirika wakipita mbele ya majeneza ya marehemu utoaji heshima za mwisho katika Hospitali ya Lugalo jijini Dar es Salaam Machi 24, 2020.*



*Baadhi ya Waombolezaji wakiwa katika majonzi wakati wa kuaga na kutoa heshima za mwisho kwa miili ya watumishi watano wa TRC waliopoteza maisha katika ajali ya treni mkoani Tanga.*




SALAMU ZA RAMBIRAMBI KUTOKA KWA MKURUGENZI MKUU TRC

Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi, menejimenti na Wafanyakazi wa Shirika la Reli Tanzania – TRC kwa masikitiko na huzuni kubwa napenda kutoa pole kwa ndugu, jamaa na marafiki wa marehemu, wafanyakazi wenzangu kufuatia msiba wa watumishi wenzetu watano (5) uliotokea tarehe 22 Machi, 2020. Namuomba Mwenyezi Mungu aendelee kuwapa faraja kipindi hiki kigumu Bwana ametoa na Bwana ametwaa Jina la Bwana lihimidiwe.

**TUTAWAKUMBUKA DAIMA**
**MASHUJAA WETU**